بسم الله الرحمن الرحيم

Muslim Youth Publication
islaahworld@gmail.com
DRTE: 01 MUHRRRAM 1431



155UE NO : 1

يا أيما الذين آمنوا اتقوا الله حق تُقاته ولا تموتنَّ إلا وأنتم مسلمون "

ZAKATUL FITR, NANI MTOAJI, NANI MSTAHIKI?

ZAKATUL FITR

Lini Zakatul fitr ilifaradhishwa

Zakatul fitr ilifaradhishwa mwaka wa pili wa Hijra, mwezi wa Shaaban.

Hukmu yake gani

Zakatul Fitr ni faradhi iliyo faradhishwa na mtume &

Amesema Abdullahi Ibn Umar & Mtume "Alifaradhisha Zakatul Fitr pishi la tende au pishi la ngano" Bukhari, Muslim

Na amesema Ibn Abbas 🐗 " Alifaradhisha Zakatul Fitr kifutio na madhambi kwa mfungaji kutokana na makosa na mambo ya kipuzi (aliyotenda mfungaji) na ni kutoa Chakula kwa maskini"

Abu Daud na Ibn Majah.

Hekima yake

- ⇒ Isafishe Makosa aliyofanya mtu pindi alipokuwa amefunga ndani ya Ramadhani.
- Maskini wasaidike mchana wa Iddi na wasipate kuomba ama kutaabika kwa kukosa chakula cha kusherehekea.

Nani anapaswa kutoa?

Kila muislamu, mume kwa mke, mchanga, kwa mkubwa - aliyefunga na ambaye hakufunga (kwa sababu za kufahamika kisheria) tajiri kwa faqiri (aliye na uwezo ama na ziada ya chakula).

Msimamizi anatoa kwa niaba ya walio chini yake - yaani baba anatolea mke, watoto, wazazi, mfanyi kazi nk.

Wanaostahiki Kupewa ni nani?

Wakupewa Zakatul Fitr ni maskini wasiokuwa na uwezo.

Nini Chastahili Kutolewa?

Chakutolewa ni chakula kama ilivyopokelewa. Amesema Abu Saeed Khudri... Tulikuwa tukitoa zama za Mtume **#** Pishi la chakula. Kiasi

Ni pishi ya zama za Mtume **%** Na ni sawa na kilo mbili na gramu kumi. Kwa kutoa shaka, kilo mbili na nusu. Chakutolewa ni chakula kilichozoelewa mjini.

Wakati wa Kutolewa

Wakati bora ni asubuhi ya Swala ya idd. Vile vile, inajuzu kutoa kabla ya idi kwa siku moja au mbili

Kutoa baada ya swala iddi ni makosa, na haihesabiwi kuwa ni zakatul fitr bali ni sadaqa.

Ibn Abbas "Mwenye kutoa kabla ya swala inaswilhi kama zakatul fitr na mwenye kutoa baada ya swala ni sadaqa kama nyinginezo"

Bila shaka, sote tuna haja iliyowazi ya kutwahirishiwa Saumu zetu. Tufanye himma kusimamisha faradhi hii.

Twaomba Allah .. Atutakabalie saumu, swala, visimamo sadaqa,dua, zaka na kheri nyinginezo.

الله اعلم Aliyekamilika ni Yeye Allah



FOR ONLINE COPY , OTHER BENEFICIAL MATERIAL OR CONTACT

http://uislamu.wordpress.com